

**WELEKEO WA MVUA KATIKA ENEO LA BONDE LA PANGANI KWA KIPINDI
CHA MWEZI OKTOBA 2024**

1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua katika eneo la bonde la Pangani kwa kipindi cha mwezi Oktoba 2024.

Kwa kawaida, maeneo ya bonde la Pangani yanayopatikana katika mikoa ya Tanga, Arusha, Manyara na Kilimanjaro, hupata mvua za Vuli kuanzia mwezi Oktoba hadi Disemba kila mwaka. Maeneo hayo yanatarajiwa kuendelea kupata mvua katika kipindi cha mwezi Oktoba 2024.

**2.0 MWELEKEO WA MVUA KATIKA ENEO LA BONDE LA PANGANI KWA
KIPINDI CHA MWEZI OKTOBA 2024**

Katika kipindi cha mwezi Oktoba 2024, maeneo ya bonde la Pangani yanatarajiwa kuwa na hali ya ukavu kwa ujumla katika maeneo mengi, isipokuwa wiki ya kwanza na wiki ya tatu maeneo hayo yanatarajiwa kuwa na mvua nyepesi.

Jedwali namba 1 na kielelezo namba 1 hapo chini, vinaonesha utabiri wa mtawanyiko wa mvua kwa kila wiki, katika kipindi cha mwezi Oktoba 2024 kwa maeneo yanayopatikana katika eneo la bonde la Pangani.

Jedwali 1: Utabiri wa mtawanyiko wa mvua katika eneo la bonde la Pangani, katika kila wiki ya mwezi Oktoba 2024


BONDE	WIKI YA KWANZA	WIKI YA PILI	WIKI YA TATU	WIKI YA NNE
PANGANI	Mvua nyepesi katika maeneo machache(hususani kusini mwa bonde la Pangani)	Hali ya ukavu kwa ujumla	Mvua nyepesi katika maeneo machache(hususani kusini mwa bonde la Pangani)	Hali ya ukavu kwa ujumla

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe: met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(IMETHIBITISHWA - ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)



Kielelezo 1: Utabiri wa mvua kwa kipindi cha kila wiki ya mwezi Oktoba 2024 katika eneo la bonde la Pangani

Utabiri huu umetolewa Leo: 30/09/2024.

Na: MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe: met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(IMETHIBITISHWA - ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)